TANGAZO LA SERIKALI Na. 721 la tarehe. 16/8/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmshauri ya Wilaya ya Muheza.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmshauri ya Wilaya ya Muheza;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"mhudumu" maana yake ni mtu anayehudumia wateja katika baa, hoteli, mgahawa, mama lishe au baba lishe;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"soko" maana yake ni eneo au soko lililotengwa na linalomikiwa na Halmashauri kama soko;

"stendi" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo hii itajumuisha pia kituo cha kupaki malori na vituo vingine vidogo vya kupakia na kushusha abiria vya Halmashauri;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri; na

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada na ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

5. Mtu anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada na ushuru utakuwa ni kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi Saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au wakala kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

Utoaji wa stakabadhi za

7.-(1) Ada au ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, utalipwa kwa Halmashauri au kwa Wakala

malipo

ambaye atatoa stakabadhi ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(2) Kila mlipa ada au ushuru atakuwa na wajibu wa kudai na kuhakiki stakabadhi ya malipo kulingana na kiasi cha fedha alicholipa.

(3) Haitakuwa utetezi chini ya Sheria Ndogo hii kwa mtu kudai kuwa amelipa ada au ushuru lakini hakupewa stakabadhi ya kielektroniki.

Ukusanyaji wa madeni

8.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za wadaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Halmashauri baada ya kupata idhini ya Mahakama itakuwa na mamlaka ya kuuza mali za mdaiwa kwa njia ya mnada baada ya siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa.

(4) Halmashauri baada ya kupata kibali cha Mahakama itakuwa na uwezo wa kuuza mali zilizokamatwa ambazo zinaweza kuharibika kwa haraka kabla hazijaharibika.

(5) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni hii, Halmashauri kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, itatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa kwa uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Uteuzi wa wakala

9.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa

viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii; na

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Ulipaji wa gharama za kuhifadhi mzigo au chombo kilichokamatwa

10.-(1) Halmashauri itatoza kiasi cha asilimia tano (5%) ya thamani ya chombo kilichobeba mzigo kwa kila siku kwa mzigo ulioshikiliwa baada ya kukamatwa ukisafirishwa bila ya kulipa ada au ushuru.

(2) Chombo au mzigo husika usipokuwa umelipiwa kwa muda wa siku saba, Halmashauri itauza mzigo au chombo hicho kwa njia ya mnada ili kufidia gharama zake.

Mamlaka ya afisa mwidhiniwa

11. Bila kuathiri masharti yoyote ya Sheria Ndogo hii, afisa mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi Saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii

Makosa

12. Mtu atakuwa anatenda kosa endapo-

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;
(c) atamzuia Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ushuru na zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri; au
(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;
(f) atashindwa, atadharau, atakaidi au kukataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii;
(g) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha

kutengeneza au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri; au

(h) atatumia chombo chochote kile kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada.

Adhabu

13. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti yoyote ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu vyote.

Kufifilisha kosa

14. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kinyume na Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

SEHEMU YA KWANZA

Ada ya ukaguzi wa ramani na vibali vya ujenzi

| Namba | Aina ya Ada kwa Viwanja Vilivyopimwa au ambavyo havijapimwa | Kiasi cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya ukaguzi wa ramani | (a) 30,000/= kwa nyumba za makazi ya kawaida (viwanja vidogo na vya kati) |
| | | (b) 50,000/= viwanja vikubwa na majengo ya biashara |
| | | (c) 120,000 viwanja na majengo ya taasisi binasfi na magharofa na minara ya simu |
| | | |
| 2. | Vibali vya ujenzi | 200,000/= kwa jengo la ghorofa |
| | | 500,000/= kwa majengo ya taasisi binafsi na viwanda |
| | | 120,000/= majengo ya biashara |
| | | 70,000/= majengo ya makazi |
| | | 500,000/= minara ya simu |
| | | 500,000/= vituo vya mafuta |
| | | 300,000/= karakana |
| 3. | Faini kwa wasio na vibali | 300,000/= hadi 1,000,000/= |

SEHEMU YA PILI

Ada ya nyumba za kulala wageni

| Namba | Aina ya Ada | Kiasi cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Wageni waliolala (watoa huduma lazima wawaorodheshe wageni kwenye kitabu na watoe taarifa sahihi) | 10% ya gharama za malazi |
| 2. | Faini kwa udanganyifu | 300,000/= hadi 1,000,000//= |

SEHEMU YA TATU

Ada ya machinjio na ukaguzi wa nyama mnadani na machinjioni

| Namba | Aina ya Ada na Ushuru | Kiasi cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ada na Ushuru wa mifugo mnadani | |
| a. | Ng'ombe | 3,500/= kwa ng'ombe mmoja |
| b. | Mbuzi | 1,500/= kwa mbuzi mmoja |
| c. | Kondoo | 1,500/= kwa kondoo mmoja |
| d. | Nguruwe | 3,500/= kwa nguruwe mmoja |
| e. | Ada ya kibanda /eneo katika mnada wa mifugo | 20,000/= hadi 40,000/- kwa mwezi au kama itakavyoamuliwa na Halmashauri mara kwa mara |

SEHEMU YA NNE

Ada ya vizimba au vyumba sokoni

| Namba | Aina ya Kizimba | Kiwango cha ada kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Matunda na mboga | 500/= |
| 2. | Magunia | 500/= |
| 3. | Vizimba vya kuuzia kuku | 500/= |
| 4. | Nafaka | 500/= |
| 5. | Chai na chakula | 500/= |
| 6. | Bucha | 500/= |
| 7. | Vizimba vinavyozunguka soko | 500/= |
| 8. | Tumbaku na chumvi | 500/= |
| 9. | Vyoo vya watu binafsi | 500/= |
| 10. | Maeneo ya wazi sokoni | 300/= |
| 11. | Vyumba/stoo ndani ya soko | 40,000/= hadi 100,000/- kutegemeana na ukubwa au kama itakavyoamuliwa mara kwa mara |

SEHEMU YA TANO

Ushuru wa stendi, kuegesha magari yanayoingia sokoni, mnadani na gulioni

| Namba | Aina ya Gari | Kiwangoc Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Basi kubwa la abiria 50 na kuendelea | 2,500/= kwa siku |
| 2. | Basi lenye ukubwa wa kati (linalobeba abiria 49 na wasizidi 30) | 2,000/= kwa siku |
| 3. | Basi dogo (haisi) | 1,500/=kwa siku |
| 4. | Teksi | 500/= kwa siku |
| 5. | Mkokoteni | 300/= kwa siku |
| 5. | Magari binafsi yasiyo ya biashara | 200/= kwa siku |
| 6. | Gari dogo la mizigo (chini ya tani 7) | 2,000/= kwa siku |
| 7. | Gari kubwa zaidi ya tani 7 | 2,500/= kwa siku |

SEHEMU YA SITA

Ushuru wa kulaza Magari

| Namba | Aina ya Gari | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | magari madogo ya watu binafsi | 2,500/= kwa siku |
| 2. | magari makubwa ya watu binafsi | 4,000/= kwa siku |
| 3. | mashine na mitambo ya ujenzi wa barabara | 5,000/= kwa siku |

SEHEMU YA SABA

Ada kwa watoa huduma za tiba asilia na wauzaji dawa za jadi

| Namba | Aina ya Huduma | Kiasi cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Waganga wa jadi | 30,000/= kwa mwaka/ 2,500 kwa mwezi |
| 2. | Taasisi | 30,000/= kwa mwaka |
| 3. | Wauzaji wa dawa za kienyeji | 300/= kwa siku 9,000 kwa mwezi |

SEHEMU YA NANE

Ada ya mbao za matangazo na matangazo ya biashara

| Namba | Aina ya Huduma | Kiasi cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mita 1 ya eneo la mraba la kila bango la viwanda/mashirika binafsi | 3,000/= |
| 2. | Biashara za kati (vituo vya mafuta, nyumba za wageni, hoteli) | 10,000/= hadi 30,000/= |
| 3. | Biashara ndogo zenye mabango na zisizo na mabango | 5,000/= |
| 4. | Yanayong'aa usiku ukiondoa yaliyoainishwa katika sehemu ya 1 | 50,000/= hadi 100,000/= |
| 5. | Aina ya matangazo ya maandishi yatatozwa katika maeneo yote ya biashara | 2,000/= |
| 6. | Matangazo yabiashara kwa kutumia vipaza sauti / muziki | 15,000/= kwa siku |

SEHEMU YA TISA

Ushuru wa mazao ya misitu

| Namba | Aina ya Huduma | Kiasi cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mkaa | 1,000 kwa gunia |
| 2. | Mbao | |
| | Urefu chini ya ft 10 [ft 0-9] | 300/= kwa kwa kila mbao |
| | Urefu zaidi ya futi 9 [ft 10 na kuendelea] | 500/= kwa kila mbao |
| 3. | Kuni | 500/= kwa ujazo wa mita 1 ya ujazo |
| 4. | Nguzo | 100/= kwa nguzo moja |
| 5. | Fito | 100/= kwa ujazo wa mita 1 ya ujazo |
| 6. | Asali | 100/= kwa lita |
| 7. | Nta | 500/= kwa kilo |
| 8. | Kibali cha kukata/kuvuna mti | 1,000/= kwa mti mmoja |

SEHEMU YA KUMI

Ushuru wa Bodaboda

| Namba | Aina ya Huduma | Kiasi cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa bodaboda kwa mzunguko wa siku nzima | 300 kwa siku |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

Ada ya kukodisha ukumbi wa Halmashauri

| Namba | Aina ya Huduma | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Ukodishaji ukumbi kwaajili ya semina za mashirika na miradi | 70,000/= hadi 100,000/= kwa siku |
| 2. | Matumizi ya ukumbi kwaajili ya asasi za kiraia | 70,000/= kwa siku |
| 3. | Matumizi binafsi | 70,000/= kwa siku |
| 4. | Kukodisha viti | 200/= kwa kiti |

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

Ada ya kukodisha magari na mitambo ya Halmashauri/ushuru wa bima

| Namba | Ukodishaji Magari na Mitambo |
|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Viwango vitakavyotamkwa na Halmashauri mara kwa mara | |
| 2. | Ushuru wa bima | 2.5% ya makusanyo |

SEHEMU YA KUMI NA TATU
Ada ya ukaguzi wa afya

| Namba | Aina ya Huduma | Kiasi cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba za starehe, baa na vilabu vya pombe za kienyeji | 20,000/= kila mwaka |
| 2. | Nyumba za kulala wageni | 20,000/= kila Mwaka |
| 3. | Maduka ya bidhaa | 20,000/= kila Mwaka |
| 4. | Nyumba za kutengeneza na kuuzia vyakula na nyama choma | 20,000/= kila Mwaka |
| 5. | Ukaguzi wa maombi ya kufungua biashara | 10,000/= kila Mwaka |
| 6. | Ukaguzi wa viwanda vikubwa | 100,000/= kila Mwaka |
| 7. | Ukaguzi wa viwanda vya kati na karakana | 50,000/= kila Mwaka |
| 8. | Ukaguzi wa viwanda vidogo | 20,000/= kila Mwaka |
| 9. | Masuala ambayo hayajatajwa na yanahitaji ukaguzi | 10,000/= kila Mwaka |
| 10. | Fomu ya Afya | 2,000/= kwa kila mtoa huduma kwa mwaka |

SEHEMU YA KUMI NA NNE
Tozo za Afya

| BIASHARA NA HUDUMA | AINA YA TOZO/ADA | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ada ya usafi kwa mwezi (Shilingi) | Ada ya ukaguzi kwa mwaka (Shilingi) | Kadi ya afya kwa mwaka (Shilingi) | Ada ya kukagua ramani ya jengo (Shilingi) | Ada ya fomu ya kupima afya kwa mtu Shilingi) | Ada ya utupaji taka kwa tani (Shilingi) | Adhabu kwa kila kosa moja (Shilingi) |
| Kaya | 2,000 kwa kila Mwezi | | | | | | |
| Mashine za kusaga nafaka | 10,000 kwa mwezi (2500 kwa wiki) | 20,000 | 10,000 | | | | |
| Nyumba za kulala wageni | 5,000 kwa mwezi | 20,000 | 10,000 | | | | |
| Hotel | 15,000 kwa mwezi | 20,000 | 30,000 | | | | |
| Vituo vya mafuta (taka za kawaida) | 5,000 | 20,000 | 30,000 | | | | |
| Viwanda (taka za kawaida) | 15,000 | 20,000 | 30,000 | | | | |
| Godauni na stoo kubwa | 10,000 | 20,000 | 30,000 | | | | |
| Bank/posta | 5,000 | 20,000 | 30,000 | | | | |
| Zahanati, Maabara, | 5,000 | 10,000 | 10,000 | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kituo cha Afya, Duka la dawa na Tiba asili (taka za kawaida) | | | | | | | |
| Mama/Baba lishe | 200/= kwa siku | 3,000 | 10,000 | | | | |
| Mgahawa | 10,000 kwa mwezi | 10,000 | 10,000 | | | | |
| Karakana (gari/pikipiki) (taka za kawaida) | 10,000 kwa mwezi | 20,000 | 10,000 | | | | |
| Maduka ya rejareja | 5,000 | 10,000 | 10,000 | | | | |
| Maduka ya jumla | 5,000 | 20,000 | 30,000 | | | | |
| Vizimba/meza za soko | 100 kwa siku ilipwe mara moja kwa wiki | | | | | | |
| Baa/Grocery | 5,000 | 10,000 | 10,000 | | | | |
| Kumbi za starehe | 10,000 | 20,000 | 30,000 | | | | |
| Ofisi | 5,000 | 10,000 | 10,000 | | | | |
| Taasisi za watu binafsi | 5,000 | 20,000 | 30,000 | | | | |
| Maeneo mengine ya biashara | 5,000 | 10,000 | 10,000 | | | | |
| Ujenzi | | | | 30,000 | | | |
| Kupima afya | | | | | 1500 | | |
| Kutumia dampo/dimbwi la maji taka la Halmashauri | | | | | | 20,000 | |
| Huduma ya kusombewa taka ngumu tripu moja | | | | | | 100,000 | |
| Usimamizi wa utekelezaji wa sheria | | | | | | | 50,000 - 250,000 |
| Kibali cha kubeba Maji Taka | | | | | | 20,000/= | |

SEHEMU YA KUMI NA TANO

Ada ya usajili wa teksi na bodaboda na daladala zinazozunguka Muheza

| Namba | Aina ya Huduma | Kiasi cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Usajili wa teksi | 20,000/= |
| 2. | Usajili wa daladala | 20,000/= |
| 3. | Usajili wa bodaboda | 5,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA SITA

Ada ya kibali cha shughuli za utamaduni

| Namba | Aina ya Huduma | Kiasi cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Disko siku za sikukuu na au siku yoyote ya juma | 5,000/= kwa siku |
| 2. | Tiba za jadi | 10,000/= kwa mwaka |
| 3. | Michezo na sanaa za maonyesho, ngoma, sarakasi, michezo ya kuigiza | 2,000/= kwa siku |
| 4. | Shughuli za sanaa za ufundi au uchoraji picha za rangi na vinyago | 1,000/= kwa onesho |
| 5. | Vikundi vya sanaa za maonyesho na sanaa za ufundi | 10,000/= kwa mwaka |
| 6. | Kucheza mchezo wa pool table | 10,000/= kwa mwaka |
| 7. | Kuendesha promosheni katika baa au hoteli | 15,000/= kwa siku |
| 8. | Sehemu za makumbusho au za kihistoria kwa mtu mmoja | (a) 1,000/= mtu mzima raia<br>(b) 25,000/= mtu mzima asiye raia<br>(c) 15,000/= mwanafunzi kutoka nje ya nchi<br>(d) Bure- mwanafunzi wa ndani ya nchi |
| 9. | Kuendesha utafiti wa masuala ya kale | (a) Raia – 50,000/=<br>(b) Asiye raia – 200,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA SABA

Usajili wa vikundi vya kijamii

| Namba | Aina ya Huduma | Kiasi cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Wanaosajiliwa chini ya maendeleo ya jamii | 20,000/= |
| 2. | Wanaosajiliwa chini ya idara nyingine za Halmashauri | 30,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA NANE

Ada ya ukaguzi wa Biashara

| Namba | Aina ya Huduma | Kiasi cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Malipo yote ya leseni yatalipwa kwa Halmashauri kabla Afisa Afya hajatoa leseni mpya au ya zamani | 10,000/= italipwa kwa leseni mpya |
| | | 10,000/= kwa leseni za zamani |
| 2. | Afisa Afya atakapofanya ukaguzi | 2,500/= |

SEHEMU YA KUMI NA TISA

Ada ya uzoaji maji machafu [Cesspit Emptying Charges]

| Namba | Aina ya Huduma | Kiasi cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Uzoaji maji machafu [Cesspit emptying charges] kwa ajili ya biashara, viwanda au majengo ya taasisi. | 150,000/= |
| 2. | Uzoaji maji machafu [Cesspit emptying charges] kwa ajili ya nyumba za makazi malipo haya yatafanyika kabla ya kutoa huduma kwa Halmashauri au wakala wake. | 80,000/= |

SEHEMU ISHIRINI

Ada ya Fomu ya vipimo vya Afya

| Namba | Aina ya Huduma |
|---|---|
| 1. | Kila mtu anayefanya kazi kwenye maeneo yanayoshughulika na vyakula au mazingira hatarishi atalazimika kulipa shilingi elfu mbili (2000) kwa Halmashauri kwa ajili ya vipimo kabla ya kupatiwa hati inayothibitisha afya yake. |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 12)*

**FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA**

Mimi .........................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MIMI MWENYEWE mbele ya........................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kwamba tarehe ..........ya mwezi .................. Mwaka................ nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kanuni ya ……..ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Niko tayari kulipa kiasi cha ada au ushuru na faini ninayodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo Tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka ……
Jina: .....................................................
Saini: ....................................................

MBELE YA:
Jina……................................................
Wadhifa: ..................................................
Saini: .................................................. Tarehe: ...............................................

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkuatno wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 29/7/2022 na Lakiri jiyo ilibandikwa mbele ya:-

DR. JUMAA MOHAMED MHINA,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Muheza*

ERASTO JEROME MHINA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Muheza*

NAKUBALI,

**L.S**

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (Mb.),
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*,